

UTARATIBU WA KUFUATA WAKATI WA KIPINDI CHA MPITO KUTOKA KWENYE KUTUMIA MFUMO WA  
LOIS WA ZAMANI KWENDA KWENYE MFUMO WA LOIS MPYA

Utangulizi

EWURA imezindua mfumo mpya wa leseni (License and Order Information System). Mfumo unarahisisha kuomba leseni katika huduma za umeme, mafuta , gesi asilia na maji . Vile vile mfumo unatumika kuomba mabadiliko ya bei katika sekta za maji na umeme na kwa kupokea malalamiko kwa wateja pale wanaohitaji kufanya hivyo.

Mfumo mpya wa LOIS umeboreshwa na kuongezewa vipengele vipya muhimu vinavyofanya mfumo kuwa rahisi kutumia.

1. Ni rahisi kujisajili na kutumia mfumo.
2. Usajili unafanyika kwa haraka sana, na unapata nywira (neni la siri) kupitia barua pepe au ujumbe mfupi.
3. Mfumo unakupa namba ya malipo (control number) kupitia ujumbe mfupi au barua pepe
4. Unaweza kupata taarifa za maendeleo ya maombi yako kwa uwazi moja kwa moja toka kwenye mfumo.
5. Mfumo umerahisisha mchakato wa kuomba leseni, ha hii inaongeza ufanisi kushughulikia maombi na kupata leseni kwa wakati uliopangwa.
6. Mfumo unakuwezesha kuomba leseni popote pale ulipo penye mtandao wa internet.

**MAOMBI YALIYO KATIKA MFUMO WA ZAMANI:** Kama umeshafanya maombi katika mfumo wa zamani na bado hayakamilika, tafadhali wasiliana na ofisi za EWURA kupitia barua pepe support@ewura.go.tz au kwa kupiga simu ya bure 0800110030 kisha taja kumbukumbu namba ya maombi yako ( reference number) na utapewa mrejesho wa hatua ambayo leseni yako imefikia.

**KUHUISHA LESENI ILIYOKWISHA MUDA WAKE:** Kama ulishakuwa na leseni na unataka kuhuisha ( renew ) leseni yako tafadhali wasiliana na ofisi za ewura kupatiwa taarifa za kutumia kuingia kwenye mfumo mpya wa LOIS.

Kwa maelezo zaidi wasilisha kwa njia zifuatazo.

Barua Pepe: support@ewura.go.tz


Simu ya bure: 0800110030

P.O.Box : 2857, Dodoma.

**KWA MAOMBI MAPYA:** Tadhali fuata taratibu zifuatazo katika kipindi hiki ili kurahisha upatikanaji wa huduma.

Kama Unaomba Maombi mapya kwa mara ya kwanza kuanzia tarehe 4 Septemba 2019 tafadhali tumia mfumo wetu mpya wa LOIS. Fuata hatua zifuatazo ili kuingina kwenye mfumo

- i. Fungua LOIS kupitia tovuti yetu [www.ewura.go.tz](http://www.ewura.go.tz) au moja kwa moja kwenye (<https://lois.ewura.go.tz/ewura/> )
- ii. Bonyeza sehemu imeandikwa Register kama inavyooneshwa hapo chini:



The screenshot shows the LOIS (License And Order Information System) login page. The header is orange with the LOIS logo and title. Below the header is the ewura logo (Energy and Water Utilities Regulatory Authority) and a login form with fields for Username and Password. A SIGN IN button is positioned below the password field. At the bottom of the form, there are links for File Complaint, Register, and Forgot password. A red arrow points to the Register link.

- iii. Jaza taarifa zinazonitajika katika fomu itakayokuja baada ya kubofya link kisha bofya Register kama inavyoonekana hapa chini :

**ewura** **LOIS**  
License And Order Information System

### Registration Form

First Name \*

Last Name \*

User Name \*

Company / FIRM Name(Business Name) \*

TIN/Taxpayer ID \*

Email \*

Telephone

Physical Address \*

Gender \*

Select a Region \*

Select a District \*

Select a Ward \*

I'm not a robot

\* All are mandatory fields

**Register**

[Click here for registration by SMS](#)

- iv. Baada ya kujisajili , utapata ujumbe mfupi au barua pepe yenye kuonyesha neno la siri. Kwa barua pepe ingia katika barua pepe yako uliyoandika wakati wa kujisajili na utapata neno la siri (nywira) ambalo utalitumia kuingia kwa mara ya kwanza.
- v. Baada ya kuingia kwenye mfumo kutumia hilo neno la siri, mfumo utakutaka ubadilisha neno hilo na kuweka neno lingine jipya kama inavyoonyesha hapo chini, badilisha neno la siri kama inavyohitajika

**ewura**


**Welcome to EWURA**  
Dear neema,

Enter New Password

Confirm New Password

**Change Password**

vi. Baada ya hapo unaweza kuingia na kutumia mfumo kuweza kutuma maombi.



vii. Ukishaingia katika mfumo unaweza kuanza maombi kwa kubofya Apply kama inavyoonekana hapo chini



viii. Jaza fomu na kupakia(upload) nyaraka zinazohitajika katika fomu kisha wasilisha maombi yako.

Endapo utahitaji msaada wowote tafadhali wasiliana nasi kwa

Barua Pepe: support@ewura.go.tz

Simu ya bure: 0800110030

P.O.Box : 2857, Dodoma.